**RISALA YA UTII KUTOKA KWA WANANCHI WA WILAYA YA DODOMA KWA MHESHIMIWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

*Mheshimiwa Rais;*

## 1.0 UTANGULIZI

Kwa heshima na taadhima kwa niaba ya wananchi na viongozi wa Wilaya ya Dodoma napenda kuwapongeza na kuwakaribisha wakimbiza Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2018 katika Wilaya yetu wakiongozwa na **Ndugu Charles Francis Kabeho.** Wananchi wa Dodoma Mjini tunaungana na kauli mbiu ya Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2018 inayosema "***Elimu ni Ufunguo wa Maisha, Wekeza sasa, kwa maendeleo ya taifa letu,*** tunasema mjisikie mpo nyumbani**,** Karibuni sana***.***

*Mheshimiwa Rais,*

Wilaya ya Dodoma ilianzishwa mwaka 1973 na Mwaka 1980 ilipewa hadhi ya kuwa Manispaa na ilipofika tarehe 26, April 2018 ilitangazwa na Mhe: Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Jiji. Wilaya ina ukubwa wa kilomita za mraba **2,769**, ina jumla ya tarafa **4,** Kata **41**, Vijiji **18,** Mitaa **170** na Vitongoji **89.** Kwa mwaka 2018 Wilaya inakadiriwa kuwa na idadi ya watu wapatao **459,350** kati ya hao Wanaume ni **222,978** (**48.54%)** na Wanawake ni **236,372** (51.46%)

*Mheshimiwa Rais,*

Mwenge wa Uhuru katika Wilaya ya Dodoma umepata michango ya Jumla ya Tshs **28,300,000** ambapo Wananchi wamechangia Tshs **16,000,000,** Halmashauri imechangia Tshs **10,000,000.00** na Wadau Tshs **2,300,000.** Aidha Mwenge wa Uhuru umekimbizwa km **81** na umepitia miradi saba (**7**) yenye Thamani ya kiasi cha Shs **5,251,746,910.80** ambapo mradi **1** ni wa mtu binafsi miradi minne (**4)** Halmashauri ya Jiji la Dodoma, mradi **1** TARURA na mradi **1** wa JKT Makutupora.

*Mheshimiwa Rais;*

## 2.0 MIRADI YA MWENGE MWAKA 2018

Kwenye Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2018 miradi iliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru ni **7** ambapo miradi **4** imewekwa mawe ya Msingi, miradi **2** imezinduliwa, na mradi **1** umetembelewa. Miradi hiyo imegharimu kiasi cha shilingi **5,251,746,910.80** kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi **812,000,000.00** ni mradi wa Serikali kwa (VETA), dhilinhi 1,265,267,980.00 ni mradi wa TARURA, shilingi 18,313,500.00 wa JKT Makutupora, shilingi 2,263,677,374.80 VETA na shilingi 892,488,050.00 ni Halmashauri.

*Mheshimiwa Rais;*

## 3.0 MIRADI ILIYOPITIWA NA MWENGE KWA MWAKA 2017.

Katika mwaka **2017** Mwenge wa Uhuru ulipitia Miradi **6** yenye Thamani ya kiasi cha Shs **4,215,497,397.00** ambapo miradi **2** ilifunguliwa, miradi **2** iliwekewa mawe ya msingi na mradi **2** ilitembelewa. Kwa miradi iliyowekewa mawe ya msingi ni kiwanda cha zabibu cha Alko Vintages Company na barabara ya Mlimwa Ring Road (Phase I), ambapo Kiwanda cha mvinyo kimeshaanza uzalishaji na barabara imeshakamilika na inatumiwa na wananchi.

*Mheshimiwa Rais;*

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA SERIKALI KATIKA SEKTA

Katika kutekeleza agizo la Halmashauri kuongeza ukusanyaji wa mapato na kutumia mfumo wa serikali za mitaa wa ukusanyaji mapato (LGRCIS na makusanyo kufanyika kwa kutumia mashine (POS). Halmashauri ya Jiji la Dodoma Kwa mwaka wa fedha **2017/2018** imefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi **25,058,290,870** sawa na asilimia **120** ya lengo la shilingi **20,798,303,295.00.** Aidha kwa Mwaka 2018/2019 Halmashauri imejipanga kukusanyakiasi cha Shilingi **67,149,647,010.00** na kuwa na mpango wa kujitegemea ifikapo 2023 bila ruzuku kutoka Serikali kuu.

Katika kutekeleza agizo la uwezeshaji wa vijana na wanawake kiuchumi, Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa Mwaka 2017/2018 imechangia kiasi cha Shilingi **950,000,000.00** kwenye Mfuko wa Wanawake na Vijana kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani vya Halmashauri kwa ajili ya kutoa mikopo kwenye vikundi vya uzalishajimali vya Vijana na Wanawake. Kiasi cha shilingi **464,000,000.00** zimeshakopeshwa kwa vikundi **234** vyenye sifa kati ya hivyo vikundi 66 vya vijana vimenufaika na jumla ya Shs **128,000,000.00** na vikundi **168** vya Wanawake vilinufaika na jumla ya Shs. **336,000,000.00**. Shilingi **486,000,000.00** ziko katika hatua ya kugawiwa katika vikundi vitakavyokuwa na sifa baada ya uhakiki.

Katika kutekeleza agizo la upandaji miti **1,500,000** kwa kila Halmashauri nchini kila mwaka, kwa Mwaka 2017/2018 Halmashauri ya jiji la Dodoma imefanikiwa kupanda miti **562,842** katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma kwa kushirikiana na watu binafsi, taasisi za Umma, asasi za kijamii na makundi maalum Changmoto kubwa ni kipindi kirefu cha ukame.
Halmashauri ya Jiji la Dodoma imetenga eneo la msitu lenye ukubwa wa hekta **150** lililopo Mahomanyika kwa ajili ya utekelezaji wa agizo la Makamu wa Rais kuifanya Dodoma kuwa ya kijani. Eneo hili la msitu ndilo lililowekewa mpango wa kulindwa, kuhifadhiwa na kuendelezwa kwa ushirikiano kati ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS).

Katika kutekeleza agizo la Tanzania ya Viwanda Halmashauri imefanikiwa kupima viwanja **983** kwa ajili ya viwanda vyenye ukubwa wa kuanzia ekari **3-7 katika** maeneo ya Nala na Mpunguzi. Pia jumla ya viwanja **48,013** vimepimwa kwa matumizi mbalimbali kama; Makazi,biashara,Taasisi,makazi na biashara, na mashamba katika maeneo ya Mtumba, Ihumwa, Kikombo, Iyumbu, Nala, Zuzu, Itega, Nzuguni, Michese, Nkuhungu, Msalato, Mlimwa, Makulu, Miyuji, Mji wa Serikali, Uwanja wa mpira na michoro ya kina yenye jumla ya viwanja **83,056** yenye matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na makazi, makazi na biashara, biashara na huduma. Aidha viwanja **67** vimepimwa katika mji wa Serikali, kati ya hivyo **62** ni vya Mabalozi na **5** ni vya Mashirika ya Kimataifa ambavyo Mh: Rais wa Jamhuri ya Muungano amevigawa kwa Mabalozi.

Kwa kuzingatia sera ya Maji ya mwaka **2002**, huduma ya maji vijijini, kiwango cha maji kwa matumizi ya nyumbani katika vipindi vyote vya mwaka ni lita **25** za maji safi na salama kwa mtu kwa siku, kwenye umbali usiozidi mita **400** kutoka kwenye makazi ya watu na kila kituo kitahudumia watu **25.** Huduma ya maji katika maeneo ya Vijijini inatolewa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma. Kwa Mwaka 2017/2018 Halmashauri imekamilisha ujenzi wa miundombinu kwenye vijiji tisa (9) vya awamu ya kwanza ambavyo ni Ntyuka, Chididimo, Gawaye, Michese, Chigongwe, Mchemwa, Mkoyo na Chihanga, jumla ya vituo (Domestic point) **158** vimejengwa vyenye vitekeo **316** ambavyo jumla ya watu **53,471** wananufaika na huduma hiyo. Aidha kwa wakazi wa Mjini wanahudumiwa na DUWASA ambapo mahitaji ya maji kwa siku yanakadiriwa kuwa meta za ujazo **46,000** na uwezo wa uzalishaji ni mita za ujazo **60,500** hivyo kuna ziada ya mita za ujazo **14,500** kwa siku. Hivi sasa DUWASA inazalisha, kusafirisha na kusambaza maji wastani wa mita za ujazo **44,000** kwa siku. Hii ni kutokana na ufinyu wa mabomba ya kusambazia maji ili kuwafikia wananchi wote wenye uhitaji huo. Hata hivyo mamlaka inaendelea na juhudi za usambazaji na ukarabati wa miundombinu ili waweze kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Katika kutekeleza agizo la kuanzisha Jumuiya za watumiaji maji Halmashauri ya Jiji kwa mwaka 2018 imeanzisha Jumuiya za watumiaji maji **18** ambazo zimepatiwa mafunzo na kusajiliwa kama vyombo halali vya usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji katika vijiji/mitaa ya Mapinduzi, Kikombo, Gawaye, Ihumwa, Mchemwa, Chihanga, Chigongwe, Chididimo, Mbalawala, Zuzu, Michese, Nkulabi, Chisichili, Matumbulu, Hombolo, Mkoyo, Nzasa na Mahomanyika.

Katika kutimiza agizo la uanzishwaji wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeanzisha jumla ya Majukwaa **41** ya Uwezeshaji Wanawake kiuchumi katika ngazi ya Kata na **1** katika ngazi ya Wilaya. Majukwaa haya ni chombo muhimu cha kuwawezesha wanawake waweze kujadiliana juu ya changamoto, mitaji na fursa za kiuchumi zinazopatikana katika maeneo yao. Changamoto kubwa ni vikundi vingi kutokuwa na sifa ya kukopesheka.

Katika kutekeleza utoaji wa elimu bure Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa Mwaka wa 2017/2018 iliweza kupunguza tatizo la Madawati Mashuleni kwa kutengeneza na kusambaza meza **500** na viti **500** kwa shule za Sekondari, utekelezaji huu unaunga mkono ujumbe wa Mwenge unaosema " **Elimu ni Ufunguo wa Maisha Wekeza sasa kwa Maendeleo ya Taifa Letu"**

Katika kutekeleza agizo la uboreshaji wa taaluma, Halmshauri imejikita katika kuhakikisha walimu wanawajibika ipasavyo kupitia ufuatiliaji wa mara kwa mara ikiwa ni pamoja na ushirikiano wa walimu na uongozi na kufanya vikao vya wadau vya mara kwa mara ili kujadili changamoto na kuzitatua, ambapo katika Mtihani wa kidato cha nne mwaka 2017 hali ya ufaulu imepanda kutoka asilimia **64.2** kwa mwaka 2016 hadi asilimia **74.05** kwa mwaka 2017. Aidha kwa Mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi ufaulu umepanda kutoka **65%** mwaka 2016 hadi **68%** mwaka 2017.

Katika kutekeleza agizo la usafi wa mazingira Halmashauri ya Jiji imefanikiwa kusafishaji, kuhifadhi, na kutupa taka ngumu kwenye Dampo la Kisasa lililopo Chidaya lililojengwa kupitia Mradi wa TSCP, Halmashauri imefanikiwa kusomba taka tani **155** kati ya tani **305** zinazozalishwa kwa siku sawa na asilimia **66**. Aidha jiji limeendelea na utekelezaji wa agizo la Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Dodoma kuhusu kufanya usafi kila Jumamosi ya mwisho wa Mwezi na linatekelezwa ipasavyo kwa ushirikiano wa viongozi wote katika ngazi ya Mkoa, Wilaya na ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji.

Katika kutimiza agizo la Maafisa Ugani kuwa na madaftari ya Orodha ya wakulima jumla ya Kata **24** zimeshawasilisha takwimu za wakulima wao. ambapo wakulima **254,773** wamepatikana, mazao yanayolimwa ni Uwele, Mtama, Mahindi, karanga,Zabibu na alizeti. Changamoto kubwa katika kutekeleza zoezi hili ni baadhi ya mashamba ya wakulima yako mbali na maeneo ya makazi hali iliyopelekea maafisa ugani/viongozi wa maeneo husika kutembea umbali mrefu.

Kuhusu agizo la kuandaa taarifa ya hali ya kilimo cha zabibu itakayoainisha idadi ya mashamba, hali ya uzalishaji katika viwanda vya kutengeneza mvinyo, na hali ya soko la zabibu na mvinyo (Wine) ni kwamba Halmashauri ya Jiji la Dododma kuna wakulima **1,234** wa zabibu wenye jumla ya hekta **717** zinazozalisha wastani wa tani **7,933** kwa mwaka na uwezo wa uzalishaji wa mvinyo katika baadhi ya viwanda vya kukamua zabibu ambavyo ni CETAWICO lita **3,000,000**, ALKO Vitage Co. Ltd lita **1,500,000,** Bihawana Winery Company lita **60,000,** Miyuji Precious Blood Winery lita **40,000**, Veyula Mission Winery lita **60,000** na wasindikaji wadogo lita **75,000.** Changamoto kubwa ni viwanda hivyo kukosa sehemu ya kupeleka mchuzi uliokamuliwa hali iliyosababishwa na Kampuni ya TBL kupunguza kasi ya kununua mchuzi wa zabibu. Hali hii pia inapelekea kukosekana kwa soko la uhakika la zao la zabibu kwa wakulima.

Halmashauri ya Jiji imefanya ununuzi wa mbegu bora za mtama, viazi lishe na muhogo jumla ya Tani **2.3** zenye gharama ya Tsh **10,000,000.00** zilizonunuliwa na kusambazwa kwa wakulima kupitia vikundi katika Vijiji **14**, wakulima mmoja mmoja wenye uhitaji, na Taasisi za Elimu (Mashule).

Katika kutekeleza agizo la upandaji wa miti ya korosho Halmashauri ya Jiji la Dodoma ilipokea kilo **192** za mbegu za korosho. Miche **21,827** ilioteshwa na kiasi cha miche **15,631** ilisambazwa kwa wakulima **150** kwenye kata **25** na taasisi **8**.

Katika kutekeleza agizo la upigaji chapa mifugo Halmashauri ya Jiji la Dodoma imefanikiwa kupiga chapa jumla ya ng`ombe **64,933** na punda **24** sawa na **90.4%** ya lengo ambalo ni kupiga chapa ng`ombe **71,826**.Changamoto kubwa ilikuwa ni wafugaji kuhamisha mifugo kwa ajili ya kutafuta malisho kwenye maeneo mengine jambo lililosababisha kutofikia lengo kwa asilimia **100**.

*Mheshimiwa Rais;*

**5.0 MIRADI YA MAENDELEO YA WANANCHI.**

Halmashauri ya Jiji la Dodoma iliidhinishiwa kukusanya na kutumia shilingi **28,881,064,347.37** kwa ajili ya miradi ya Maendeleo, fedha zilizopokelewa ni shilingi **18,766,779,261.99.** kati ya fedha hizo shilingi **13,590,241,893.00** ni fedha za miradi ya Maendeleo zinazotokana na mapato ya ndani sawa na asilimia **72** na shilingi **5,176,537,368.90** ni fedha za ruzuku ya Serikali kuu. Sawa na asilimia **28** Aidha miradi iliyotekelezwa ilikuwa ni pamoja na ulipaji wa fidia na upimaji viwanja shilingi **9,439,819,227.00** na shilingi **3,566,832,598.46** zilitumika kwa ajili ya miradi ya Elimu, Afya, Maji na usafi wa mazingira.

Serikali imetekeleza mradi wa uboreshaji vituo vya Afya vya Makole, Hombolo na Mkonze yenye jumla ya shilingi **1,400,000,000.00,** mradi wa Kituo cha Afya Makole umekamilika na unafanya kazi, Hombolo uko katika hatua ya ukamilishaji na Mkonze uko katika hatua za awali. Kupitia mradi wa **TASAF** mabwawa **26** yamekarabatiwa, makinga maji **9,** kilimo cha bustani za mbogamboga **13** na uoteshaji wa vitalu vya miti **36** kwa gharama ya shilingi **490,728,000.00**.

*Mheshimiwa Rais;*

Katika kutekeleza agizo la Serikali la kuzitaka Halmashauri zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya kugharamia ulinzi Mashuleni Halmashauri ya Jiji la Dodoma imetenga jumla ya Shilingi **157,920,000.00** kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kulipia, gharama za ulinzi, Maji na Umeme kwenye shule zote **94** za Msingi za Umma.

Kwa Mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Jiji la Dodoma imetenga jumla ya Shilingi **2,553,512,908.00** sawa na asilimia **10** ya mapato ya ndani baada ya kuondoa fedha za “Revolving fund” kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Halmashauri ya Jiji la Dodoma inaendelea kutekeleza uboreshaji wa miundombinu mbalimbali inayotoa huduma kwa wananchi, kwa kupitia mradi wa Tanzania Strategic Cities Project (TSCP) Halmashauri ya Jij la Dodoma inatekeleza ujenzi wa Kituo cha kisasa cha mabasi ambacho kitakuwa na

uwezo wa kupaki mabasi 250, bajaji na pikipiki **300,** magari madogo **600** na maeneo maalum kwa ajili ya Machinga ndani ya kituo cha mabasi ili kutekeleza agizo la Mhe. Rais la kuwa na Machinga katika eneo la stendi.

Miradi mingine itakayotekelezwa ni kituo cha maegesho ya malori, soko, Bustani ya kupumzikia ya Chinangali, ujenzi wa **km 26** za barabara kiwango cha lami na ujenzi wa km **6.5** za mitaro ya maji ya mvua. Miradi hii kwa jumla itagharimu kiasi cha Tsh **77, 881, 955,400.34** hadi kukamilika na inategemea kukamilika mwezi Septemba, 2019.

*Mheshimiwa Rais;*

## 6.0 MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI

### 6.1 HALI MAAMBUKIZI YA VVU

Hali ya maambukizi ya VVU katika Jiji la Dodoma imeongezeka kutoka **3.9%** kwa mwaka 2017 hadi kufikia asilimia **4.1** kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na Mkoa wa Dodoma wenye kiwango cha Maambukizi ya VVU ya asilimia **5.0%.**

Katika kipindi cha 2017/ 2018 Chini ya kauli mbiu inayosema **" Mwananchi Jitambue Pima afya yako sasa"** Jumla ya watu **45,415** (Me **22,639**,Ke **22,776**) walijitokeza na kupima maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI kwa hiyari kati yao wenye maambukizi walikuwa ni **1,885**( 4.1%).
Ili kufikia malengo ya Tanzania kwamba ifikapo mwaka 2020 asilimia **90** ya watu wanaoishi na VVU wanatambua hali zao za maambukizi, mpaka sasa asilimia **90** kati yao wanatumia ARV na asilimia **90** ya wanaotumia ARV kiwango chao cha VVU mwilini kinashuka. Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeweza kushiriki katika zoezi la uzinduzi wa Kampeni ya "Furaha Yangu" na inayoongozwa na kauli mbiu " **Pima, Jitambue, Ishi,** jumla ya watu **4,754** walijitokeza, waliogundulika na maambukizi ya VVU walikuwa **110** sawa na **2.3%.**

Jumla ya wagonjwa wapya **2,365** waliogundulika kuwa na maambukizi ya VVU walianzishiwa dawa za kufubaza VVU hivyo kufikisha idadi ya **WAVIU** waliopo katika tiba kuwa **11,420** ambayo ni sawa na **90.1%** ya lengo. Dawa

zikitumika ipasavyo hupunguza kwa kiwango kikubwa maambukizi mapya ya VVU na kuboresha hali ya maisha ya WAVIU. Aidha katika kupambana na maambukizi mapya ya VVU elimu imetolewa na jumla ya kondomu 135,211 zilisambazwa katika Kata zote **41** za Jiji.

Halmashauri ya Jiji la Dodoma inashirikiana na wadau mbalimbali katika utekelezaji wa afua za mapambano dhidi ya UKIMWI. Wadau hao ni pamoja na Engender heath, HPSS,John Snow Inc.(JSI),PSI,TIENAI,ILO, CMSR, BAOBAB COMMUNITY FOUNDATION kupitia mradi wa (SAUTI), NACOPHA – KONGA kupitia mradi wa (SAUTI YETU), Sharing World Tanzania,TIKVAH HOMES,KISEDET, Bakwata, Jumuia ya Kikristo Tanzania, SORF,JHPIEGO,EGPAF, na Baylor International.

*Mheshimiwa Rais;*

## 7.0 MAPAMBANO DHIDI YA UGONJWA WA MALARIA

Chini ya kauli mbiu inayosema **"Shiriki kutokomeza Malaria kwa manufaa ya Jamii"** Halmashauri ya Jiji la Dodoma imefanya kampeni maalum ya kupambana na Malaria kwa kupulizia dawa kwenye mazalia ya mbu katika mabwawa, visima na makaro ya kuhifadhia maji machafu katika Kata **41** za Jiji la Dodoma ambapo. Jumla ya lita **1,280** za dawa zimekwisha kutumika kwa awamu ya kwanza. Pia katika kutekeleza mkakati wa kinga ya malaria kwa mama na mtoto, jumla ya vyandarua vyenye viuatilifu **12,160** vimesambazwa kwenye vituo vya huduma za afya kwa ajili ya kupewa kina mama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Hali ya maambukizi ya malaria imepungua na kufikia **0.9%** katika jiji la Dodoma ukilinganisha na kiwango cha kitaifa cha **9%** kwa mwaka 2018.

*Mheshimiwa Rais;*

## 8.0 MAPAMBANO DHIDI YA MADAWA YA KULEVYA

Chini ya kauli mbiu inayosema **"Tuwasikilize na kuwashauri watoto ili wasitumie dawa za kulevya"** Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wameendelea kutoa elimu juu ya madhara ya matumizi ya madawa ya kulevya

kwa vijana wapatao **287** (Me 128 Ke 59) wanaotumia madawa mbalimbali ya kulevya. Idadi ya vijana waliondikishwa katika Sober House ni **68.**

*Mheshimiwa Rais;*

**9.0 HATUA ZILIZOCHUKULIWA JUU YA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA.**

Taasisi ya kuzuia na kupambana na Rushwa ofisi ya mkoa kwa kipindi cha 2017/2018 kazi zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo. Taarifa zilizopokelewa katika kipindi hicho ni **150**, Kesi zilizofunguliwa ni **11**, kesi zilizoshinda **2**, kesi zinazoendelea **9** na fedha zilizookolewa ni Tsh **6,797,633,873.**Pia taasisi ilifanikiwa kufungua klabu za wapinga rushwa **64**, kuimarisha klabu **33,** kutoa semina **24,** mikutano **30,** makala **4,** vipindi vya redio ni **11** na maonesho **2** yalifanyika**.**Katika uchambuzi wa mifumo uliofanyika katika Taasisi za serikali **6**, warsha **5** na ufuatiliaji wa maazimio ya warsha **5.**

*Mheshimiwa Rais;*

**10.0 UWEKEZAJI KATIKA ELIMU**

**10.1** Halmashauri ya Jiji la Dodoma inaungana na ujumbe wa Mwenge kwa mwaka 2018 unaosema "***Elimu ni ufunguo wa maisha wekeza sasa kwa maendeleo ya Taifa letu "*** kwa kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuwekeza katika elimu, kama hatua muhimu ya kuzalisha nguvu kazi yenye ujuzi wa kusaidia Taifa katika kufikia mapinduzi ya kiuchumi yatakayoiwezesha Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ya Jiji iliitisha kikao cha wadau wa elimu ili kuhamasisha uboreshaji wa elimu na kuweza kuongeza uwekezaji kwa watu binafsi katika elimu.

**10.2 UJENZI WA MIUNDOMBINU YA SHULE**

Kwa upande wa miundombinu na vifaa vya shule za msingi, Wilaya imeendelea kuwekeza kwa kushirikisha wadau mbalimbali na kutenga fedha kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji. Kupitia programu ya **EP4R**, jumla ya vyumba **35** vya madarasa vimejengwa katika shule za msingi **5** kwa thamani ya shilingi **660,000,000**/= matundu ya choo **85**, yenye thamani ya shilingi **94,840,510/=** na nyumba **4** za walimu zenye thamani ya shilingi **217,000,000**. Katika mwaka wa huu wa fedha **2018/2019** Halmashauri imetenga jumla ya shilingi **1,469,976,000**/= kutokana na

makusanyo ya ndani kwa ajili ya kuboresha na kuongeza miundombinu ya shule za msingi. Miongoni mwa shughuli zitakazofanywa ni ununuzi wa madawati **2,650**, kukamilisha vyumba **67** vya madarasa, nyumba **13** za walimu, majengo **6** ya utawala na matundu **62** ya choo. Aidha kupitia miradi ya EQUIP jumla ya shilingi **145,000,000/=** zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa shule shikizi **2** na kumalizia maboma **2** ya madarasa.

Katika mwaka 2017/2018 Miundombinu ya shule za sekondari imejengwa ambapo Jumla ya madarasa **25** yamejengwa na kukamilika katika shule za Sekondari **11**, matundu ya vyoo **55** yamejengwa katika shule **5** Ujenzi wa hosteli **4** katika shule **4**. Sambamba na maabara **14** pia zipo katika hatua ya umaliziaji na nyingine **11** zimeanza kuendelezwa katika mwaka wa fedha 2018/19 na tunategemea maabara **25** zitakamilika.

**10.3** Kwa kuzingatia umuhimu wa sayansi katika mapinduzi ya viwanda. Shule za Msingi na sekondari zimeendelea kuwahamasisha wanafunzi wa jinsi zote kupenda masomo ya sayansi kwa njia shirikishi ikiwa ni pamoja na kuunda klabu za Sayansi na kuboresha ufundishaji wa masomo husika kwa kuwajengea uwezo walimu wa masomo hayo kwa njia ya mafunzo.

**10.4** Wilaya ya Dodoma ina jumla ya vyuo **2** vya ualimu, vyuo **6** vya Elimu ya juu vinavyotoa mafunzo katika fani mbalimbali na vyuo vya ufundi **21** vinavyowaandaa mafundi wa fani anuwai zenye mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya viwanda.

Sisi wananchi wa Wilaya ya Dodoma tumefarijika sana kwa ujio huu wa Mwenge wa Uhuru ambao ni ishara ya Utaifa na Uhuru wetu. Kwa kupitia mbio za mwenge wananchi wa Dodoma tunakupongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwezesha Makao Makuu ya Serikali kuhamia Rasmi Dodoma, kusimamia rasilimali za Watanzania kutopotea, Kusimamia miradi mbalimabali kama  Kutangazwa kwa Ujenzi wa Uwanja wa ndege Msalato, Ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo wa kimataifa kata ya Nzuguni, Ujenzi wa Ikulu Chamwino, Ujenzi wa Reli Standard Gauge, Mungu aendelee kukulinda na kukupa maisha marefu. Tunawapongeza wakimbiza

Mwenge Kitaifa kwa kazi nzuri mliyoifanya ya kukimbiza Mwenge wa Uhuru toka ulipowashwa hadi kufikia leo tarehe 05/08/2018. Tunawaombea ninyi nyote wakimbiza Mwenge na kiongozi wa mbio hizi Mungu awape nguvu na afya ili muweze kukamilisha kazi hii nzito ya Kitaifa salama.

*SISI WANANCHI WA WILAYA YA DODOMA*

*Nawasilisha*

Patrobas Katambi

**MKUU WA WILAYA DODOMA**